



ACTION2DAY PRESS

# St. Spyridon

---

*The shepherd who became a bishop*

English · Kiswahili



Long ago, young Spyridon was a humble shepherd. He loved his sheep and guided them gently. He thanked God every day for the gift of life.

*Zamani, Spyridon akiwa kijana alikuwa mchungaji mnyenyekevu. Aliwapenda kondoo wake na kuwaongoza kwa upole. Kila siku alimshukuru Mungu kwa zawadi ya uhai.*



Spyridon lived in a small, peaceful home with his wife and little daughter. They prayed together, worked hard, and shared joy even though they had little.

*Spyridon aliishi katika nyumba ndogo yenye amani na mke wake pamoja na binti yao mdogo. Waliomba pamoja, walifanya kazi kwa bidii, na walifurahia maisha.*



He always welcomed strangers. If someone was hungry, he shared his bread. He believed God's love should be shared with all.

*Daima aliwakaribisha watu wageni. Mtu akiwa na njaa, aliwapa mkate wake. Aliamini upendo wa Mungu ni wa wote.*



One day, God called Spyridon to serve at the church. The bishop blessed him and gave him a white robe. Spyridon promised to serve God and His people.

*Siku moja, Mungu alimwita Spyridon kuhudumu kanisani. Askofu alimbariki na kumpa joho jeupe. Spyridon akaahidi kumtumikia Mungu na watu wake.*



Later, he became a bishop on a small island. Even with this great responsibility, he continued to live simply and humbly.

*Baadaye, akawa askofu wa kisiwa kidogo. Hata akiwa na jukumu kubwa, aliendelea kuishi kwa unyenyekevu na urahisi.*



He walked with the people, spoke gently, and blessed them with his staff. He loved everyone like a shepherd loves his flock.

*Aliishi kati ya watu, akizungumza kwa upole, na kuwabariki kwa fimbo yake. Aliwapenda watu kama mchungaji anavyowapenda kondoo wake.*



When a drought came and crops dried, Spyridon prayed.  
Soon, gentle rain fell and the fields turned green again.

*Ukame ulipotokea na mazao kukauka, Spyridon aliomba. Mara mvua ikanyesha taratibu na mashamba yakawa ya kijani tena.*



The sick came to him for help.  
He prayed, and God healed  
them.

*Wagonjwa walimwendea kutafuta  
msaada. Aliwaombea, na Mungu  
akawaponya.*



To teach about God's power, he blessed a loaf of bread. Fire rose, water flowed, and wheat appeared — showing God's mystery and love.

*Kuonyesha nguvu ya Mungu, alibariki mkate. Moto ukatoka juu, maji yakatoka chini, na ngano ikabaki — ishara ya upendo wa Mungu.*



A farmer was about to lose his land. Spyridon gave him coins to save it, because he believed no family should suffer alone.

*Mkulima mmoja alikuwa karibu kupoteza shamba lake. Spyridon alimpa sarafu kumsaidia, kwa sababu aliamini hakuna familia inapaswa kuteseka peke yake.*



Sometimes angels visited him while he prayed. They brought peace and light.

*Mara nyingine malaika walimtembelea alipokuwa akiomba.  
Walileta amani na mwanga.*



A man stole a sheep. After seeing Spyridon's kindness, he returned it and was forgiven.

*Mtu mmoja aliiba kondoo. Alipoona wema wa Spyridon, alimrudisha na akasamehewa.*



A child died suddenly. Spyridon prayed with tears — and God brought the child back to life.

*Mtoto mmoja alikufa ghafla. Spyridon aliomba kwa machozi — na Mungu akamrudisha uhai.*



To help people across a flooded river, he walked on the water through God's power.

*Kusaidia watu kuvuka mto uliofurika, alitembea juu ya maji kwa nguvu za Mungu.*



On a ship, a storm grew fierce. He prayed, and the sea became calm.

*Akiwa ndani ya mashua, dhoruba ilianza. Aliomba, na bahari ikatulia.*



He helped enemies become friends. Peace gave him joy.

*Aliwapatanisha maadui wakawa marafiki. Amani ilimletea furaha.*



Birds and animals came to him with love — even God's creatures knew his kindness.

*Ndege na wanyama walimkaribia kwa upendo — hata viumbe vya Mungu vilijua wema wake.*




A lost traveler met him at night. Spyridon showed him the way home.

*Msafiri aliyepotea alimkuta usiku. Spyridon alimwonyesha njia ya kurudi nyumbani.*



He loved his daughter and taught her to love God and people.

*Alimpenda binti yake na kumfundisha kumpenda Mungu na watu.*



He prayed under trees and thanked God for the beauty of creation.

*Aliomba chini ya miti na kumshukuru Mungu kwa uzuri wa uumbaji.*



When he grew old, he fell asleep in peace and went to be with the Lord.

*Alipokuwa mzee, alilala kwa amani na akaenda kuwa na Bwana.*



Today, his body rests in  
Corfu. His shoes wear  
out because he still  
'walks' to help people...

*Leo, mwili wake uko Corfu.  
Viatu vyake huisha kwa  
sababu bado 'anatembea'  
kusaidia watu...*



*Painted & edited by*

## **Action2day Art Center · Nairobi**

---

Fabian Romain Lashley  
Griffins Nyangaresi Museti  
Steve Mugiraneza Rukeramihigo  
Caleb Gathii Manyera  
Abigael Nyaboke Nyakundi  
John Maina Onyango

Irene Kiviya Nduku  
Ecclesiastes Madaraka Medo  
Kristian Juma Omedo  
Maxwell Mukanga Indukule  
Angel Miriam Mlenda